

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HAILMASHAURI YA JIJILA TANGA

Telegramu: MKUU WA SHULE
Simu Na. 2642082
Mkuu wa Shule (Nyumbani) 078488909



Shule ya Sekondari Tanga Ufundi,
S.L.P 5002,
TANGA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. TTS.A.3/16/VOL.III/57

29/11/2016

NDUGU MZAZI/MLEZI WA

KIDATO CHA II & IV 2017

YAH: MWANAO KURUDI NYUMBANI KWA AJILI YA LIKIZO NDEFU, DESEMBA 2016

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu

Ndugu mzazi/mlezi, ninakutaarifu kuwa shule imefungwa rasmi tarehe **29.11.2016** na itafunguliwa siku ya Jumapili tarehe **08.01.2017** tayari kuanza masomo Jumatatu tarehe **09.01.2017**.


Kwa Wanafunzi wa kidato cha **pili** na cha **nne** watakuwa na mitihani ya Mock na Taifa mwakani (2017). Kila mwanafunzi aandaliwe sare za kushindia shuleni (shamba dress) ambayo kwa wasichana ni gauni mbili, moja rangi ya zambarau na nyingine rangi ya pinki (kama hana). Wavulana itakuwa ni suruali ya rangi ya khaki na fulana ya rangi ya kijivu yenye ukosi shingoni (maarufu kwa jina la "form six") pea mbili.

Ndugu mzazi/mlezi, hiki ni kipindi kizuri kwako kumuandalia mwanao mahitaji hayo ya shule ya muhula ujao.

Ripoti ya matokeo ya mitihani ya mwanao ya Novemba 2016 itatumwa kwako kwa njia ya posta. Tafadhali ndugu mzazi/mlezi, hakikisha unafuatilia mwenendo wa mwanao kitaaluma na kitabia. Pindi anwani yako inapobadilika tafadhali tunaomba utoe taarifa shuleni kimaandishi.

Mwisho, tunakutaarifu ndugu mzazi/mlezi, kuwa kama mwanao atalazimika kuvaa sweta shuleni kwa sababu zozote zile za kiafya au nyinginezo, sweta inayokubalika shuleni ni ile ya rangi ya **Dark Blue** yenye shingo ya V. Ni marufuku mwanafunzi kuvaa sketi fupi, au zisizo na marinda, suruali zinazobana (vimodo), vikoti/makoti/vizibao au sweta za rangi nyingine kama sare ya shule. Inasitizwa kuwa suruali chini ziwe na upana wa inchi 17 au 18, mbele ziwe na rinda mbili kila upande na mifuko ya cross, nyuma mfuko mmoja. Pia ziwe na luksi sita za kuwekea mkanda mweusi wenye kifungio cha kawaida. Simu kwa mwanafunzi hazitakiwi kabisa shuleni.

Ahsante, ninakutakia malezi na maandalizi mema.


A.W Mwakanyamale
MKUU WA SHULE

HEADMASTER
TANGA TECHNICAL SCHOOL
TANGA